JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU ATHARI ZINAZOHUSISHWA NA MATUMIZI YA MAFUTA YA KULA

**Dar es Salaam, 02 Mei 2025**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilipokea taarifa kuhusiana na uwepo wa madhara ya kiafya yanayohusishwa na kutumia mafuta ya kula yaliyotokea kwa wananchi wanaoishi Kata ya Makangarawe Mtaa wa Yombo Dovya Manispaa ya Temeke pamoja na Kata ya Vijibweni, Mtaa wa Majengo, Manispaa ya Kigamboni Dar es Salaam. Waathirika walieleza kula chakula cha aina tofauti tofauti kama vile chapati, vitumbua, maandazi, samaki wa kukaanga, viazi vya kukaanga na kupata madhara ya kiafya yanayofanana ikiwa ni pamoja na maumivu makali ya kichwa na uchovu wa mwili, maumivu ya tumbo kuharisha, kutapika, maumivu ya macho, athari za kwenye ngozi ya mwili na athari za upumuaji.

TBS ilifanya ukaguzi na kuchukua sampuli kutoka katika maduka na kaya zilizoathirika kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara. Aidha, TBS ilifanya mahojiano na waathirika na kubaini kuwa, vyakula vyote vilivyoelezwa kuleta madhara ya kiafya viliandaliwa kwa kutumia mafuta ya kupikia ya aina moja yaliyonunuliwa katika maduka ya bidhaa za chakula kwa rejareja, yaliyopo katika Mtaa wa Yombo Dovya na Mtaa wa Majengo.

Vilevile, TBS ilifanya ukaguzi kwa wasambazaji wa mafuta ya kula kwa bei ya jumla na kukuta uwepo wa madumu 99 ya mafuta ya kula yenye ujazo wa lita 20 kila moja ya aina mbalimbali ambayo taarifa kwenye kifungashio zimefutika. Aidha, madumu hayo 99 hayakuwa na lakiri halisi ya mzalishaji (unsealed jerrycans) hali ambayo inaashiria kwamba mafuta hayo yalikuwa hayajafungwa kwa mujibu wa kiwango husika cha mafuta ya kula. Baada ya ukaguzi madumu ya mafuta hayo tisini na tisa (99) yalizuiliwa kwa uchunguzi zaidi.

Aidha, TBS ilifuatilia uingizwaji wa mafuta hayo ambapo vibali vilionesha kuwa mafuta hayo yalikidhi matakwa ya ubora na usalama wakati wa uingizwaji na Kampuni ya Long Wide Traders kutoka Indonesia kupitia Bandari ya Zanzibar na kisha Bandari ya Bagamoyo kati ya mwezi Novemba na Desemba, 2024, na jumla ya madumu 7,500 ambayo ni sawa na lita laki moja hamsini (150,000) ya mafuta ya kula yaliingizwa. Baada ya ufuatiliaji huu TBS

ilijiridhisha kuwa mafuta hayo hayakuwa na tatizo wakati wa kuingia nchini kwani kiasi hicho cha mafuta ni kikubwa na kwamba athari ambazo zingetokea zingehusisha idadi kubwa zaidi ya waathirika kama yangekua na changamoto yoyote wakati wa uingizwaji.

Hata hivyo, matokeo ya uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara kwa sampuli 99 zilizochukuliwa katika mafuta yaliyozuiliwa yanaonesha kuwa ni mafuta ya mawese (*Palm Olein*) ambayo baadhi yake, sampuli 14 (14%) hayakidhi kiwango cha ubora na usalama cha Tanzania kwa kuwa na kiasi kikubwa cha *Free Fat Acid* (sampuli 12 (12%), *Peroxide value* (sampuli1 (1%) na kubadilika kwa *Fatty acid composition* (sampuli 1 (1%) kwa mujibu wa viwango vya Tanzania (TZS 559:2018) – *Tanzania Standard – Palm Olein Specification*). Aidha, matokeo ya uchunguzi wa mabaki ya sampuli ya mafuta yaliyochukuliwa kutoka katika moja ya kaya za waathirika yalionesha uwepo wa kemikali aina ya *(E, E) -2,4-Decadienal na E-2 Decenal.*

Uwepo wa kiasi kikubwa cha Free Fatty Acids (FFA), *Peroxide Value ni kiashiria cha mafuta ya mafuta ya kula kuharibika. Aidha, (E, E) -2,4-Decadienal ambayo ni Polyunsaturated fatty aldehyde, ambayo ni mojawapo ya mazao (by-products) ya mafuta ya kula yaliyoharibika.* Kwa mujibu wa taarifa za kisayansi, kemikali hii inaweza kusababisha madhara kwa binadamu kama vile kuumwa kichwa, kuwashwa macho na ngozi, malengelenge (bristers), kichefuchefu, kutapika, kuwashwa koo, kizunguzungu, na hata kusababisha kifo kutegemeana na kiasi kilichoingia mwilini.

Aidha, taarifa za kisayansi zinaonesha kuwa *(E, E) -2,4-Decadienal na E-2 Decenal* haziwezi kupatikana katika mafuta ambayo bado hayajatumika kupikia na ikiwa zitapatikana kwenye mafuta hayo ni kwa kiasi kidogo hasa pale ambapo mafuta yamekaa muda mrefu katika mazingira yasiyo sahihi kwa utunzaji wa mafuta ya kula. Kemikali hizi hutokea kwenye mafuta yaliyotumika kukaangia chakula kwa muda mrefu katika joto kali au matumizi ya kurudia kupikia/kukaangia mara kwa mara (recycled). Hivyo, matokeo haya yanahusianishwa na mafuta kutumika kupikia katika joto kali.

Aidha, uuzaji wa mafuta ambayo hayana lakiri ya mtengenezaji ni kosa kisheria, hivyo wahusika watachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Sura 130 kifungu cha 27.

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka
**Meneja Uhusiano na Masoko**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023